

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam
Tarehe 14 Julai 2007**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishekh
Ally Salum
Bakari Dafa
Elaine Baker
Faustin Gessabo
Filbert Mbecha
Hamadi Hatibu Bwaja
Iddi Salehe
Ismaili Saidi
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kassim Bakari
Kelvin Mbawala
Kibwana Mohammad Msiga
Paulo Atibu Hatibu
Rashidi Saidi Karanji
Shabani Ramadhani
Sudi Saidi
William Samweli

Akaunti ya Benki

Ali Saidi Mohamed aliarifu kuwa aliwasiliana na serikali za mitaa jitegemee kupata barua ya utambuzi ya UWABA kwa NMB benki. Alhamis Mejah, Elaine na Juma walikwenda benki na wakafanikiwa kufungua akaunti, ambapo Elaine aliweka Tsh 11,000 kama kianzio. Akaunti namba ni 2052300909. tuna kadi ya benki ikiwa na picha tatu na sahihi mbili zitatakiwa kuchukua fedha.

Barabara zilizo kwenye mpango wa ujenzi.

Meja, Elaine, Juma, Abdallah na shukuru walikwenda Carl Bro Associate. Wakala wa barabara ya Nelson Mandela alhamisi. Maelezo ya mkutano huu yako kwenye nyaraka tofauti. Kati ya meta 45, ni meta 6 tu zimetengwa kwa waenda kwa miguu, wapanda baiskeli na vyombo vingine vya usafiri visivyotumia injini, pamoja na barabara za matengenezo, pia inapitika na magari barabara imedhaminiwa kwa asilimia 100 na umoja wa ulaya (EU)

UWABA imepokea jibu la barua yetu kutoka CPC, mtaalam mshauri wa ujenzi wa barabara ya kilwa barua inasema kwamba kuna meta 3 kila pande ya barabara ambayo inaweza kutumika kwa waenda kwa miguu na wapanda baiskeli. Wanachama walielezea hisia zao kuhusu hili kwani barabara ya kilwa ina idadi kubwa ya waenda kwa miguu na wapanda baiskeli.

TANROADS haijajibu barua zetu. Hatua ifuatayo ni kuandika maoni yetu kwa TANROADS na EU kwa suala la barabara ya Nelson Mandela.

Msafara wa baiskeli

Elaine aliarifu kuwa Godfrey wa CHABADA aliwapigia simu AALOCOM ila hajakutana na yeyote. Elaine aliwapigia simu ijumaa ila hakuna aliyekuwepo kuhudhuria kikao cha msafara kilichopangwa kufanywa leo. Hivyo kiliahirishwa.

Kwa sababu tuna akaunti benk inaaminika itakuwa rahisi kwa mchango kwa ajili ya msafara.

Mbunge kupanda Baiskeli Bungeni

Gazeti la Mtanzania lilionyesha picha ya mbunge wa Ilala akiwa amepanda baiskeli kwenye kurasa za mbele. Nakala hiyo ilieleza kuwa mbunge huyo alisema upandaji baiskeli ni njia mojawapo nzuri ya usafiri ambayo inatumika kwenye nchi zilizoendelea na viongozi. Wajumbe waliamua kumtumia barua ya hongera kwa kupanda baiskeli na kumwomba awe mgeni rasmi kwenye msafara wa baiskeli.

Sanduku la barua

Meja alifanikiwa kuangalia kwenye sanduku na kupata barua kutoka CPC. Alisema atawasiliana na Juma ili kupata nakala ya funguo kwa ajili ya UWABA.

Mpango Madhubuti wa Usafiri Dar es Salaam

Hatujapata jibu lolote kutoka halmashauri ya jiji la Dar es Salaam JICA au chuo cha usafirishaji Dar es Salaam, kwa barua zetu za kuomba kumuishwa kama wadau katika kupanga.

Ofisi

Wanachama walitoa mchango kwa ajili ya kuanzisha ofisi / kituo cha maelezo, hivyo jumla ya michango sasa ni Tsh 20,000 ambazo zimenunuliwa kwenye kitabu cha akaunti cha Juma. Elaine alitangaza kuwa Mathew cogan amekubali kuchanga dola 100 ambazo ni Tsh 120,000. wanachama walielezea furaha yao kwa kiwango hicho cha fedha. Pamoja na mchango wa Joseph lake wiki iliyopita Tsh 50,000 toka kwa Elaine, Jumla kuaa imekuwa Tsh 240,000 inayohitajika kwa mwaka wa kwanza wa kodi. Tunatakiwa kuendelea kuchangia gharama za kupaka rangi, kununua samani na kununua gata ili kupata fedha za mwaka ujao.

Jumanne alisema kwamba yuko mtu mwingine anayefuatilia ofisi hiyo hivyo hivyo tunatakiwa kulipa mapema kwa mwenye nyumba sofia. Alisema atahakikisha anapata risiti ili kuthibitisha kuwa tumelipa kodi ya mwaka mmoja.

Mengineyo

Wanachama zaidi walichukua vitambulisho vyo na kuchangia Tsh 500 kama gharama za utengenezaji. Jumanne alihifadhi orodha ya michango.